

JUKUMU LA VYOMBO VYA KIELEKRONIKI KATIKA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA  
FASIHI YA WATOTO

Harriet K. Ibala  
Chuo Kikuu cha Moi

**Ikisiri**

Makala hii itaangazia jukumu la vyombo vya kielektroniki, kama vile runinga, redio na mtandao katika kukuza na kuendeleza fasihi ya watoto. Hizi ni kazi za fasihi zinazowasilishwa na watoto wenyewe au na watu wazima, wakilenga watoto kama hadhira yao. Katika makala hii, watoto watachukuliwa kuwa na maana ya wale walio na umri wa hadi miaka kumi na mitano. Kati ya mambo yatakayotiliwa maanani katika makala hii ni tanzu za fasihi zinazohusika, kiwango cha lugha inayotumiwa, urefu na ujumbe unaowasilishwa katika kazi za watoto ikilinganishwa na viwango mbalimbali vya watoto wanaolengwa. Vigezo hivi ni baadhi ya mambo muhimu ambayo huwawezesha watoto kufaidika kutokana na kazi zinazowalenga kama wapokezi. Athari za kazi hizi vilevile zitachunguzwa ili kusaidia katika kuweka mipaka inayostahili katika utunzi, uandalizi na uwasilishaji wa kazi za watoto.